

**OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

Anuani ya Simu "TAMISEMI" DODOMA
Simu Na: +255 26 2321607
Nukushi: +255 26 2322116
Barua pepe: ps@tamisemi.go.tz



*Mji wa Serikali – Mtumba,
Mtaa wa TAMISEMI,
S.L.P. 1923,
41185 DODOMA.*

TAARIFA KWA UMMA

**MKANGANYIKO ULIOJITOKEZA KUHUSU LUGHA YA KUFUNDISHIA NA
KUJIFUNZIA KWA WANAFUNZI WA SEKONDARI**

Ofisi ya Rais -TAMISEMI na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeona mijadala na taarifa mbalimbali zisizosahihi kuhusu ufundishaji wa somo la Kingereza na kufungia matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye shule za Sekondari.

Mijadala na taarifa hizo zimewasilishwa kwa namna tofauti, jambo ambalo limesababisha mkanganyiko kwa jamii na kumekuwa na upotoshwaji ambao umesambaa ndani na nje ya nchi juu ya matumizi ya lugha ya Kiswahili na Kingereza kwenye shule za Sekondari nchini.

Hivyo, Serikali kupitia Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeona vyema kutoa ufafanuzi kuhusu taarifa hizo kuwa Serikali katika mabadiliko ya mitaala ya mwaka 2010 na Sera ya Elimu na mafunzo ya mwaka 2014 hayakufanya mabadiliko kwenye lugha ya kufundishia na kujifunzia katika Shule za Sekondari.

Sera ya Elimu na mafunzo ya mwaka 2014 katika ukurasa 37 inabainisha kuwa “Kwa sasa Lugha za kufundishia na kujifunzia katika Elimu ni Kiswahili na Kiingereza” Aidha, Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 imebainisha kuwa;

- a) Lugha ya kufundishia Elimu ya Awali na Msingi ni Kiswahili; na
- b) Lugha ya Kiingereza hutumika kufundishia katika shule za Sekondari.

Aidha, tamko namba 3.2.20 la Sera hiyo limebainisha kuwa, “Serikali itaendelea na utaratibu wa kuimarisha matumizi ya Lugha ya Kiingereza katika kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote za Elimu na Mafunzo.

Serikali inasisitiza ufundishaji wa kozi ya Kiingereza kwenye Shule za Sekondari kwa undani ili kuwapa wanafunzi fursa ya kufanya mazoezi ya kutosha ya kutumia lugha ya Kiingereza na kuimarisha umahiri wao wa matumizi ya lugha hiyo.

Pamoja na Lugha ya Kiingereza kutumika kufundishia Shule za Sekondari, Serikali itahakikisha lugha ya Kiswahili na lugha nyingine za kigeni zinafundishwa kwa ufasaha na ufanisi katika ngazi zote za Elimu na mafunzo nchini sawa na tamko namba 3.2.17 la Sera ya Elimu na mafunzo ya Mwaka 2014.

Tunatoa wito kwa wananchi wote ndani na nje ya nchi kutambua kwamba, hakuna mabadiliko yaliyofanyika kuhusu ufundishaji wa somo la Kiswahili katika Shule za Sekondari. Kiswahili ndiyo lugha yetu ya Taifa na hilo halina mabadiliko na ni lugha iliyopewa hadhi ya kutumika katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Nchi zilizo Kusini mwa Afrika pamoja na Umoja wa Afrika.

Nchi yetu inaendeleza jitihada zaidi za kufundisha walimu wengi wa Kiswahili ili waweze kufundisha lugha hii adhimu na kukieneza kiswahili duniani kote.

Imetolewa na



Nteghenjwa Hosseah
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Ofisi ya Rais –TAMISEMI
14.01.2023